

## **Azimio la Watoto kuhusu Usalama Barabarani**

Ni kwa nini maelfu ya watoto huuwawa na kujeruhiwa katika ajali za barabarani kila siku kote ulimwenguni? Ni kwa sababu hatua zinazochukuliwa hazitoshi. Enyi viongozi wetu, mnahitaji kusikiliza na kuchukua hatua.

Sisi ni watoto. Huenda tukawa na sauti siku zijazo, lakini kwa sasa ni wajibu wenu kutusaidia. Hatua zinapaswa kuchukuliwa haraka iwezekanavyo, la sivyo, watoto wengi hawatakuwa na nafasi ya kufika umri wa wakuweza kujisemea.

Nyinyi viongozi na watu wazima mnapaswa kutusaidia kwa kuunga mkono wito huu wa kuchukua hatua kuhakikisha watoto wote wanasafiri barabarani kwa usalama.

Sote tunastahili kuweza kusafiri kwenda shule na kurudi kwa usalama. Barabara lazima ziwe salama ili watoto waweze kutembea kuelekea shuleni. Tunahitaji njia za miguu na za baiskeli zilizo salama na matuta ya kudhibiti kasi ya magari. Vilevile tunahitaji vivukio vya miguu salama ili tuweze kupokea elimu bila uwoga ama hatari ya kujeruhiwa.

Tunatoa mwito kwa magari yanoyowabeba watoto popote pale kote ulimwenguni yawe salama. Magari yote na mabasi yanapaswa yawe na mikanda ya usalama. Watoto wanaobebwa kwa pikipiki ni lazima wavae kofia za usalama. Tunafahamu kuwa kuvaa kofia za usalama au kujifunga mikanda ya usalama kunaokoa maisha.

Kuendesha gari au pikipiki ukiwa mlevi ni hatari. Kuendesha gari kwa mwendo wa kasi vile vile ni hatari. Watu wanaowajali watoto hawapaswi kufanya mambo kama haya. Hakuna mtu anayefaa kufanya hivyo. Maafisa wa usalama wanapaswa kutulinda na kumzuia yeyote yule atakaye endesha gari kwa mwendo wa kasi au akiwa mlevi. Inabidi usalama usisitizwe kila wakati – tunapojumuika na wanajamii, tunapoenda kucheza ama kuelekea shuleni.

Sheria lazima zitungwe, maoni yasikizwe na hatua zichukuliwe kuhakikisha barabara zi salama kwa watoto wote kote ulimwenguni.

Kwa hivyo twatoa mwito kwenu, viongozi wa mataifa, kuhusisha hatua dhidi ya usalama barabarani katika malengo mapya ya maendeleo duniani. Popote pale tunapoishi tunataka na kutarajia usalama barabarani kwa marafiki wetu, jamaa zetu na kwa sisi wenyewe.

Mara nyingi sauti zetu hazisikiki kwa kuwa sisi ni watoto tu. Kwa hivyo tunaomba mtusaidie kwa kuchukua hatua. Ikiwa mtatupatia barabara zilizo salama sasa, tutakua tunaweka mfano mzuri kwa vizazi vingi vijavyo. Tafadhali sikilizeni na kuchukua hatua. Itanusuru maisha ya watoto.

Linda Maisha ya Watoto  
kwa usalama barabarani